TANGAZO LA SERIKALI NA. 846 la tarehe 11/10/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8 (1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA KINANGWE'ELI YA MWAKA, 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga eneo la Kinangw'eli ya mwaka, 2024.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na ya kina katika eneo lililoainishwa kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya Itilima.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VB225 yenye majira – nukta 582174.000MS, 9679108.000KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kufuata mto Sola hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VB224 yenye majira – nukta 584130.000MS, 9678719.000KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS132$^{0}$02'44''MS kwa umbali wa kilomita 4.465 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VB223 yenye majira – nukta 587525.000MS, 9675667.000KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini- Magharibi katika uelekeo wa KS204$^{0}$29'31''MG kwa umbali wa kilomita 1.901 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BA86 yenye majira – nukta 586695.300MS, 9673845.700KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS224$^{0}$15'58''MG kwa umbali wa kilomita 0.639 hadi kwenye alama ya

mpaka ya upimaji namba VB222 yenye majira – nukta 586179.000MS, 9673316.000KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS228$^{0}$08'05''MG kwa umbali wa kilomita 2.343 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba
VB221 yenye majira – nukta 584359.000MS, 9671685.000KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ293$^{0}$43'11''MG kwa umbali wa kilomita 2.475 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VB184 yenye majira – nukta 581993.000MS, 9672703.000KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ338$^{0}$44'12''MG kwa umbali wa kilomita 4.166 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VB183 yenye majira – nukta 580413.000MS, 9676666.000MS; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ36$^{0}$47'47''MS kwa umbali wa kilomita 2.910 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
2 Oktoba, 2024

DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*